**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 16 Juni, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Bajeti kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2025/2026.

## III. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

51. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Huko nyuma kwa nia njema viongozi wetu wa nchi walianzisha programu maalumu ya kufanya usafi kwa pamoja katika maeneo mbali mbali ya miji kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi. Jambo hili lilikuwa zuri ambalo liliweka utamaduni mzuri na kupunguza taka na hata maradhi ya kuambukiza katika mitaa yetu.

(a) Je, ni changamoto gani iliyoifanya Serikali kushindwa kuisimamia programu hiyo muhimu kwa afya zetu.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuboresha agizo hili ili wananchi waweze kuendeleza utamaduni huu mzuri.

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha hulipwa kwa mwaka kwa wasafishaji wa nje (outsourcing firm) katika kuiweka miji yetu safi na salama.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

174. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Kuna jitihada kubwa ambazo mwenza wa Mhe. Rais Mama Maryam Mwinyi amekuwa akizipambania kiuchumi na kijamii.

Kwa kiasi gani jitihada zake zimekuwa na matokeo chanya kwa jamii.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

56. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Taasisi nyingi za dini na Asasi za Kiraia zinakumbwa na changamoto kubwa, vikwazo vingi na urasimu katika mchakato wa kupata misamaha ya kodi wanapopokea vifaa au misaada kutoka nje ya nchi. Hali hii inasababisha vifaa hivyo kukaa bandarini kwa muda mrefu na kutozwa ada za kuhifadhi ambazo mara nyingi hawawezi kuzilipa.

(a) Kwa kiwango kipi Serikali inalitambua tatizo hili na juhudi gani imechukua kulitatua.

(a) Je, kwa takwimu ni misamaha ya kodi ya kiasi gani hutolewa kwa mwaka hapa Zanzibar kwa Taasisi za Dini na Asasi za Kiraia.

(b) Je, ni kwa namna gani misamaha hii ya kodi inayotolewa inawafaidisha wananchi wa Zanzibar.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

85. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Watunzi wetu wengi wa nyimbo za taarabu asilia wamefariki na wengine kuzeeka.

Je, Serikali imelifikiria vipi suala hili kwa kuwa ni sehemu moja ya utalii na utamaduni wa nchi yetu.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

227. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa utaratibu wa kugundua na kuibua vipaji kwa vijana tangu wakiwa wadogo umeleta mafanikio makubwa kwa nchi za magharibi.

(a) Je, utaratibu na muongozo kama huo unafanyika vipi katika maskuli yetu na hata kupitia ngazi za wazazi nyumbani.

(b) Ni yepi matarajio ya utaratibu huu katika kuibua walimu mafundi na wanasayansi wakubwa katika taifa letu.

301. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2022, shehia ya Wawi na Wara ni miongoni mwa shehia zenye watu wengi. Hata hivyo, shehia hizo hazina Skuli za Msingi na hivyo wananchi wake hutumia skuli zilizopo katika shehia jirani.

Je, ni upi mpango wa Serikali wa kujenga skuli kwenye shehia hizo.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

104. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ni yepi matarajio ya kuanzishwa kwa majukwaa ya wanawake katika ngazi za shehia nchini.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

94. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

(a) Kwa kiasi gani maeneo ya hifadhi ya bahari yanasimamiwa ipasavyo.

(b) Kwa sasa ni changamoto gani zinaathiri usimamizi wa hifadhi za bahari wakati tukiadhimisha na kusherehekea siku ya wanawake duniani kwa hatua kubwa.

**<u>Wizara ya Afya:</u>**

55. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Moja ya ugonjwa unaoathiri sana wananchi wetu hivi sasa ni ugonjwa wa kisukari. Ugonjwa huu hupelekea wananchi wengi kuathirika na hata kupelekea vifo wanapokosa tiba ya haraka.

(a) Ni ipi takwimu ya wagonjwa wanaosumbuliwa na ugonjwa wa kisukari Zanzibar.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kutoa huduma kwa ngazi ya shehia ili kuweza kutibu tatizo hili.

(c) Je, Serikali ina madaktari bingwa wangapi wa kuweza kusaidia kupambana na ugonjwa huu wa kisukari.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

83. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Pamoja na juhudi za Serikali za kujenga maegesho ya kisasa na kujaribu kuweka utaratibu mzuri wa malipo katika maegesho hayo, kumekuwa na changamoto ya malipo pale unapokwenda kuweka gari kwenye maegesho yote ya Mji Mkongwe.

Je, kuna utaratibu gani wa malipo kwa wanaotumia maegesho ya Mji Mkongwe.

101. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Ni jitihada zipi za dharura ambazo Wizara yako imezichukua baada ya takwimu kuonesha kuwepo kwa upungufu wa watalii kwa takriban asilimia 1.6 mwaka huu.

IV. **HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili na Kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2025/2026.

Zanzibar,
16 Juni, 2025.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA LA
WAWAKILISHI, ZANZIBAR.